


EDSON MKONGE
Ugonjwa wa
korona, 666 na
ulimwengu mpya
wa kisayansi.



ONYO

©2021 Haki zote zimehifadhiwa hairuhusiwi kunakili au kuiga kitabu hiki bila idhini ya mwandishi. Unaweza nifatilia katika mitandao ya kijamii kama vile; YOUTUBE MKONGE TV

GOOGLE; edsonmkonge.blogspot.com

Na email; edsonsosthenes86gmail.com

Cell; +255 714367701 or +255 755010857

DIBAJI

Mambo yanayotokea katika ulimwengu wetu wa leo hatuna budi kuyafikiria sana kwani kila mahali ulimwenguni tunaona ghasia na misukosuko pamoja na milipuko ya magonjwa ya kutisha kama huu ugonjwa ulioibuka hivi karibuni yaani korona [uviko 19/covid 19] bahari, maziwa na mito kuchafuliwa, miti inaangamizwa, mabadiliko makubwa ya hali ya hewa [climatic change] na watu maelfu kwa maelfu kukimbia nchi zao ili kuondokana na hatari, maafa, njaa, vita na vifo.

Si ajabu kwamba watu wale wanaoaminiwa kuwa manabii waliyatabiri mambo hayo yote kama vile mtume petro alivyosema “nasi tunalo lile neno la unabii lililo imara zaidi ambalo mkiliangalia kama taa ing’ayo mahali penye giza mwafanya vema [2 Peter 1; 19] Edson mkonge mwandishi wa kitabu

hiki amezungumzia masuala yahasuyo imani, kuhusu matukio yanayoendelea hivi sasa ulimwenguni hasa ugonjwa wa korona na kuelekea ulimwengu wa kidijitali.

Kile ambacho mungu amesema katika maandiko matakatifu ya manabii wake, kwani wakati ujao unatisha na kukatisha tamaa, lakini liko tumaini Kwa wanaomwamini Mungu na maandiko yake. Matumaini hayo ya maisha bora, yenye amani na raha yang'aa mioyoni mwao watakaokisoma kitabu hiki.

UTANGULIZI

Maendeleo makubwa makubwa na ya haraka haraka pamoja na mataifa kushindana katika mambo makuu ya kisayansi za kivita, biashara na teknolojia nyinginezo katika siku zetu hizi, Kwa kipindi cha millenia iliyopita mengi ya mambo makuu katika maisha ya watu hayakubadilika. Kazi zilifanywa kwa mikono ya mwanadamu au kutumia wanyama waliovuta magari yaliyokuwa na magurudumu ya miti.

Lakini tangu miaka 200 iliyopita mabadiliko makubwa yametokea. Uvumbuzi wa mitambo na matumizi ya mawasiliano yanayotokana na mwendo msogeo wa elektroniki duniani kote hubadilisha maisha ya wakaaji wa dunia yetu kila baada ya saa. Gurudumu la historia limeonekana kuzunguka haraka sana, mambo mengi yaliyopita

ya kuigwa miaka elfu moja iliyopita sasa yanaonekana yamepitwa na wakati, kwa vile binadamu leo anadhani elimu ya kisayansi italeta amani, heri na maisha bora maishani.

Ujuzi na werevu wa kisayansi wa binadamu umeongezeka

mara.....

.....